SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.20 NO. 2 2021
DOI: 10.51984/JOHS.V20I2.1768

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Malezi Ya Watoto Enzi Za Wazanzibari Wa Kale

Mohammed Amhammed Mohammed Ali Taher

Idara Ya Lugha Na Taaluma Za Kiafrika, Kitivu Cha Sanaa, Chuo Kikuu Cha Sebha, Libya

**Keywords:**
Watoto
Mama
Chakula
Zanzibar
siku

**ABSTRACT**

Maandalizi ya malezi ya watoto enzi za wazanzibar wa kale yalianza mapema mara mwanamke anapochukuwa uja uzito. Mjamzito aliandaliwa mambo maalumu kama chakula chake , nguo , sehemu maalumu ya kukaa ili ajifungue salama na kuanza kumlea mwana. Naye mwana aliyezaliwa alikuta ameshaandaliwa mambo yanayomhusu na hupokelewa kwa dua na shangwe toka kwa wanafamilia na wengine. Alipelekwa madrasa kujifunza kusoma kurani tukufu na elimu nyingine za maadili ya kiislamu ambazo ndizo zilizokuwa msingi mkuu wa kurekebisha maadili yake. Pamoja na haya alifundishwa kivitendo kuheshimu wengine katika jamii kwa kadri ya hadhi zao . Alipelekwa shule kujifunza elimu za mazingira na sayansi mbali mbali pamoja na lugha za kigeni na sanaa mchanganyiko ili kumjenga kimaarifa na kumwandaa kuitumikia jamii. Watoto walipobaleghe walipelekwa jandoni, kwa watoto wa kiume, na unyagoni kwa watoto wa kike. Huko walifunzwa namna ya kukabiliana na mabadiliko yaliyojitokeza katika miili yao na namna ya kuishi katika jamii wakiwa watu wazima tayari kuanzisha familia pindi muda utakapowadia. Malengo makuu ya malezi haya yalikuwa kumtayarisha mtoto kuishi maisha ya maadili mema katika jamii na kutoa mchango wake kwa kadiri ya nafasi yake katika jamii husika.

# تربية الطفل عند قدماء الزنجباريين

محمد إمحمد محمد على الطاهر

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية الأداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
اليوم
الطفل
الأطفال
الاكل

**الملخص**

بدأ الزنجباريون القدماء استعدادهم الكامل لتربية أطفالهم الجدد عندما تحمل المرأة بمولودها، فيجهز الأقارب للمرأة الحامل كل مايلزمها في فترة حملها من الطعام، والشراب، واللباس، والدواء، إلى أن يحين موعد ولادتها، وهذا التجهيز الكامل للحامل هو تسهيلا لها؛ لإنجاب مولودها بكل يسر،وسهولة، وسلامة، ومن دون مشقة، أو عناء، أو تعب، فيستقبل أفراد الأسرة، والأقارب مولودهم الجديد بالدعاء، والثناء، والحمد، والشكر لله سبحانه وتعالى على هذه النعمة التي تعد في الحقيقة أمنية عظيمة لكل أب، وأم٬يترعرع الطفل بين أحضان أمه وأبيه، ثم يرسل بعد أن يشتد عوده،ويقوى ساعده إلى إحدى مدارس التعليم القرآني؛ ليتعلم في قاعاتها الدراسية ٬ القرآن الكريم،والعلوم الإسلامية، ثم يتعلم مكارم الأخلاق، والأدب الرفيع؛ لأن هذين الأمرين هما أمران أساسيان في تهذيب سلوك الطفل، ونقله من مرحلة إلى أخرى، ومن ثم يتلقى دروسا علمية، وعملية تساعده في فهم أمور الدنيا، والطريقة الصحيحة للاختلاط بالناس، وكيف يعامل طبقات الناس الموجودة معه في مجتمعه بحسب منزلهم الاجتماعية، وصلة قرابته منهم٬مع الأيام، والشهور، والسنين، يكبر الطفل شيئاً فشيئا، ثم يرسل إلى مدارس المراحل المتقدمة من التعليم، فيتعلم العلوم التطبيقية، والإنسانية، واللغات الأجنبية ؛ من أجل تقوية معارفه،وتوسيع إدراكه، وبناء قدراته، وتطوير مهاراته، وإعداده إعدادا جيدا لخدمة مجتمعه، ووطنه٬عندما يبلغ الطفل سن المراهقة، ينقل إلى أماكن خاصة للتدرب، ولتلقي كل مايلزمه بخصوص فهم هذه المرحلة الحرجة من

*Corresponding author:
E-mail addresses: moh.taher@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 18 May 2021 - Received in revised form 27 October 2021 - Accepted 15 December 2021*

عمر الإنسان، فيوضع الأولاد في جهة، والبنات في جهة أخرى،فيتعلم الذكور، والإناث الطريقة الصحيحة للتعايش مع مكونات المجتمع تعايشا يسوده الوئام،والوفاء، والاحترام، والتقدير'الأهداف الرئيسية من هذه التربية :(1) - إعداد الطفل إعدادا جيدا؛ لضمان عيش حياة كريمة في مجـتمعه (2) - إسهام الطفل إسهاما كبيرا بقدر جهده، وطاقته، وإمكاناته في المجتمع الذي ينتمي إليه.

**Utangulizi**

Maelezo hii tafuta yaliyomo katika makala hii yamekusudiwa kutoa taswira fupi lakini angavu ya mojawapo ya vipengele vya maisha ya wakaazi wa Zanzibar ya kale. Neno kale laweza kumtatiza msomaji na kuwaza kale ile ya mbali sana, laa, kale hii ni ile ya nyakazi za mwanzo wakoloni wa uUlaya walipofika Zanzibar na kuanzisha mifumo mipya kama vile kujenga maskuli na kuleta mfumo mpya wa elimu .

Makala imelenga kumjuvya msomaji yaliyojiri wakati ule katika malezi ya wana wa kizanzibari nyakati hizo na jitihada zilizotumika katika kumwandaa kukabiliana na maisha pindi akuwapo na kujiandalia mustakbali mwema.

Maneno na nyimbo alizoimbiwa mwana huyu vililenga sio tuu kumnyamazisha na kilio chake bali pia kupanda mbegu ya kupenda kujifunza na zaidi ilikuwa ni ahadi za mbembelezaji mwana kumtunuku mwanawe kila kilicho bora kitakachomsaidia maishani.

**KUJIFUNGUA NA MALEZI YA MTOTO**

**Mama Mjamzito**

Tangu zamani, mwanamke mwenye ujauzito wa miezi tisa, anakwenda kukaa na kusubiri kujifungua nyumbani kwao. Hasa iwapo hiyo ni mimba ya mwanzo. Mwanamke huyo hutakiwa aende kwa mama na baba, shangazi au bibi. Endapo wazee hao wameshafariki, aghalabu huwa anakwenda kwa wakwe zake; yaani, mama na baba wa mume.

**Nyumbani Kwao**

Akiwa nyumbani kwao, au kule kwa wakwe zake, mambo kadhaa hufundishwa. Mafunzo anayopatiwa, humsaidia katika kufahamu namna ya kumlea mwana na kumtunza. Hivyo, hufunzwa namna ya kujinadhifisha yeye mwenyewe, kumnadhifu mtoto, nguo na vyombo vyake.

Kadiri ya siku za kujifungua zinapokaribia kufika, huitwa shekhe kuja kumzungua. Yaani, kuja kumuombea dua ili ajifungue salama.

**Vitu Vya Kutayarisha.**

Zamani mjamzito wa Zanzibar alikuwa anatafutiwa mtama ima kutoka kondeni au ulinunuliwa dukani. Mtama huo ulisafishwa vizuri hadi uwe safi kabisa. Halafu, huanikwa kidogo. Hatimaye hutwangwa hadi uwe unga.

Dalili za kujifungua zinapochomoza, huchotwa unga kidogo na kupikiwa uji. Waswahili wanaamini kuwa uji huzidisha 'uchungu' wa kujifungua kuongezeka na kumfanya mjamzito kuzaa kwa haraka. Unga mwengine unaobakia huwekewa mwanamke huyo baada ya kujifungua.

Matayarisho mengine ni pamoja na kutafutiwa asali, pilipili manga, mdalasini, karafuu, tangawizi, uzile na kuku.

Halikadhalika, baadhi ya familia hununua kabisa nguo za mtoto na kuziweka kwa jirani. Sababu ni kwamba iwapo mtoto atafariki zile nguo zitabaki huko ili zisizidishe huzuni ya mama. Hata hivyo, familia nyengine hazinunui nguo mpaka mtoto azaliwe.

**Siku Ya Kujifungua**

Wajawazito wa Zanzibar husuka nywele karibu ya siku za kujifungua. Mara tu baada ya mama kujifungua, babu au baba wa mtoto humshika mwanawe sikio la kulia na kumuadhinia. Hao wakikosekana, mwanamme yeyote aliyepo hutenda tendo hilo.

**Utoaji Wa Jina La Mtoto**

Mara nyingi baba ndiye anaetoa jina la mtoto wa mwanzo. Hata hivyo, baadhi ya familia nafasi hiyo hupewa babu au bibi. Utaratibu mwengine unaotumika ni kwamba baba na mama wa mtoto, au familia zao hupendekeza majina na kupigiwa kura. Kila jina hufichwa kwenye kipande cha karatasi na kutakiwa mtoto yeyote aliyepo achague kikaratasi kimojawapo. Baadaye karatasi hufunguliwa, na jina liliyomo ndilo jina la mtoto analopewa. Utaratibu wa siku ya kutoa jina hutafautiana kutoka familia moja na nyengine. Wengine hutoa jina siku ya uzawa wake na wengine hutoa siku ya saba ya kuzaliwa.

**Chakula Cha Mama Wa Mtoto**

Chakula cha mama aliyejifungua (aliyezaa) ni uji wa mtama au sembe uliopikwa kwa asali na sukari, pamoja na kutiwa pilipilimanga nyingi, tangawizi na uzile (bizari nzima). Utaratibu wa kunywa ni mara tatu au nne kwa siku kama hivi ifuatavyo.

- Asubuhi: Anakunywa uji, mikate ya maji na asali.
- Mchana: Anakunywa supu ya kuku na wali wa maji laini (ubwabwa). Supu inatiwa pilipilimanga kidogo, tangawizi na uzile .
- Jioni: Anakunywa tena uji na kitu chochote.
- Usiku: Hunywa uji, mkate na supu ya kuku. Kwa desturi, supu ya kuku huwa anakunywa kwa siku saba. Baadaye hupata ruhusa ya kula chakula chochote. Hata hivyo, mzazi huendelezwa kupewa uji kwa wiki mbili au zaidi, inategamea mama mtoto anavyopenda. Lakini pia uchaguzi wa chakula inategemea na hali ya maisha yao. Halikadhalika, endapo mama maziwa hayatoki, anakunywa supu ya pweza au uji wa unga wa muhogo na hapo maziwa yatatoka.

**Kumtizama Mama Na Mtoto**

Zamani watu walikwenda kumtizama mama aliyejifungua wakati wa asubuhi, mchana na jioni. Lakini siyo mara nyingi kutizama usiku. Hata hivyo, jamaa wa ndani wanaruhusiwa kumtizama mzazi wakati wowote. .

Kwa desturi ya Wazanzibari, yule anaekwenda kumtizama mtoto na mama huchukua zawadi yeyote. Kama vile, nguo ya mtoto, nepi, sabuni ya kuogea mtoto, sabuni ya kufulia, sukari, unga na kitu chochote.

Pia mara nyingine mtoto hupewa pesa mkononi au zinawekwa chini ya mto wa kulalia (mtoto).

**Kumfichua Mtoto**

Mtu anapokwenda kumuona mtoto kwa mara ya kwanza, kwa desturi ya Wazanzibari huwa hawezi kumuona mpaka amfichue. Yaani atowe pesa

kidogo. Aghalabu, watu wanaotakiwa kumfichua mtoto ni watu wa familia kama vile kama mjomba,shangazi ndugu na kadhalika. Hata hivyo, endapo itashindikana kutoa pesa, basi mtu anaweza kutoa zawadi yoyote.

**Kuanguka Kitovu**

Katika hali ya kawaida, kitovu cha mtoto huanguka kwa siku ya tatu, sita au saba. Inategemea na hali ya afaya ya mtoto na ukatwaji wa kitovu.

Kitovu kinapoanguka kinachukuliwa na kutiwa ndani ya pamba au kipande cha kitambaa. Halafu hupewa bibi mzalia mama wa mtoto au bibi yake mzalia baba. Bibi huyo hukichukua na kwenda kukizika kwao katika bustani au kwenye shamba lao.

**Mama Mtoto Au Mzazi**

Zamani, baada ya mama kujifunga, hutayarishiwa chumba chake maalumu. Katika chumba hicho huwekwa kitanda cha kamba na gao la moto chini ya kitanda kwa siku zisizopungua saba hadi ishirini. Lengo la kutenda hivyo ni kufanya mwili wa mama usipate baridi. Halikadhalika, ni kwa nia ya kulisafisha tumbo la mzazi.

Aidha, Waswahili wa Zanzibar wanayo desturi ya kumkanda mama mazazi kila asubuhi kwa muda wa wiki moja au zaidi. Anakandwa kwa maji ya moto na majani ya mbarika na anapakwa mafuta ya alizeti au ya nazi .

**Mtoto Aliyezaliwa (Kuogeshwa**

Zamani, mtoto aliyezaliwa (mtoto wa siku moja) anaogeshwa chumbani siyo bafuni au uani. Mtoto anapoogeshwa ni lazima pawe na chetezo chenye makaa ya moto, mafuta ya alizeti na habasoda au ubani wa kufukiza. Chetezo kinatiwa habasoda au ubani na huku mtoto anaogeshwa. Baadaye anapakwa mafuta ya alizeti kwa muda wa siku 40 au zaidi.

**Chakula Cha Mtoto**

Zamani tangu siku ya kwanza mtoto alinyonya titi la mama tu hadi kufikia miezi mitatu au zaidi. Mara nyengine mtoto hupewa maji yaliyochemshwa. Hasa nyakati za asubuhi na jioni wakati mtoto anapotaka kuogeshwa. Huchotwa maji kidogo kutoka kwenye sufuria inayochemshiwa maji ya kumuogeshea mtoto na kunyweshwa kabla hajaanza kuogeshwa.

Endapo mama hana maziwa kifuani, mtoto hunyweshwa maziwa ya ng’ombe au mbuzi. Mara nyengine, hupikiwa uji au mbatata na kupondwapondwa. Halikadhalika, huweza kupondewa matunda kama vile papai, ndizi mbivu na embe mbivu.

**Kuanzia Miezi 9 Mpaka Miaka Mwili**

Mtoto anayonya titi la mama asubuhi, jioni na usiku. Anakula ubwabwa (wali laini) ndizi mbichi zilizopondwa na supu ya samaki au nyama , nyama au samaki matunda maji, maji ya matunda, mkate wa boflo unaotiwa siagi na jamu pamoja na chai. Hata hivyo, chakula hichi hutafautiana kutoka familia moja na nyengine kulingana na utafauti wa hali ya maisha.

**Akiki**

Zamani siyo sana mtoto kufanyiwa akiki. Zile familia zilizofanya, ilikuwa inafanyika siku ya saba ya uzawa wake au siku ya kumi na nne au siku ya ishirini na moja.

Kama mtoto ni mwanamme, huchinjiwa mbuzi wawili na nyama inatolewa sadaka. Endapo mtoto ni mwanamke baba anachinja mbuzi mmoja na nyama inatolewa sadaka. Hata hivyo, mara nyingi nyama hupikwa pale mahala mtoto alipo na watu mbalimbali hualikwa kuja hapo kwa ajili ya kula nyama hiyo. Mifupa huwa haivunjwi na hukusanywa na kisha hufukiwa kwenye shimo. Inaaminiwa kuwa ikivunjwa, mtoto naye huweza kuvunjika viungo kadhaa ukubwani kwake pale anapofikwa na ajali.

**Kumuachisha Mtoto Kunyonya**

Katika visiwa vya Zanzibar, kuna njia tofauti za kumfanya mtoto aache kunyonya. Njia ya kwanza ni kumpelekamtoto kwa bibi au shangazi au ndugu wa karibu wa baba au mama na kukaa naye kwa siku kadhaa mpaka asahau kunyonya. Baadaye anarudi nyumbani.

Njia ya pili ni kwambamama huweka pamba katika titi na humtisha mtoto. Mtoto akiona tu huwa anaogopa na kulia. Baada ya siku chache anasahau na hivyo huacha kunyonya.

Njia ya tatu, ni kwamba titi la mama hupakwa shubiri kidogo. Mtoto akinyonya, anapata hisia za uchunguuchungu na hivyo, anaacha kunyonya mara moja.

**Kumbembeleza Mtoto**

Mtoto wakati anapolia, hubembelezwa kwa nyimbo mbalimbali. Mara nyingi huchaguliwa nyimbo za kumuombea dua na zenye ujumbe mzuri. Kwa sababu Waswahili husema kuwa “wimbo mbaya habembelezwi mtoto”. Mfano:

Oooh ! Ooooh! Oooooh!
Mtoto wangu mzuriii,
Nikupeleke skuliii,
ufunzwe mambo mazuriiii
Oooh! Oooh! Ooooh!
Usilie usilieee
Ukaniliza na miyeee

Machozi yako yawekeee
Nikifa unililieee
Oooh! Oooh! Ooooh!.
Kile kidau kijachooo
Hamkosi mna changuuu
Mna mkufu wa kitooo
Kadiri ya shingo yanguuu
Kuupata siuvaiii
Wala simpi mwenzanguuu
Nitampa mama yanguu
Msiri wa mambo yanguuu
Oooh! Oooh! Oooh!

Mambo Anayofanyiwa Mtoto Mchanga

Zamani,mtoto mchanga ilikuwa haachwi peke yake. Lazima mtu akae naye endapo mama anataka kuodoka labda kwenda jikoni au chooni. Endapo hakuna mtu wa kukaa naye basi, mama huweka chini ya mto wa mtoto ndimu, kisu kidogo. Sababu ya kufanya hivyo, walisema kuwa inazuia shetani kumfikia mtoto.

Vile vile, mtoto hasa wa kike, hupakwa wanja aonekane ana sura mbaya ili kumkiga na macho ya watu wenye hasadi.

Mara nyengine mtoto hufungwa kitambaa cha rangi nyeusi mkononi; hasa mkono wa kushoto. Ndani ya kitambaa chenyewe kuna kipande cha mvuje. Harufu ya mvuje husaidia katika kuwakimbiza mashetani waovu wasimkurubie mtoto. Halikadhalika, asubuhi na jioni, chumba cha mtoto kinafukizwa kwa ubani na habasoda. Nia ni kukimbiza wadudu waovu kama vile mashetani.

Desturi ya zamani ya Wazanzibari, mtoto alikuwa hapakwi podari au kitu chenye harafu nzuri. Hupakwa mafuta ya alizeti au ya nazi tu.

**Siku 40 Ya Kuzaliwa**

Zamani ilikuwa inafanyika sherehe ya kutimiza siku arubaini tangu kuzaliwa kwa mtoto. Ilikuwa ikifika asubuhi ya siku ya arubaini, mtoto anatiwa kwenye ungo. Ndani ya ungo kuna bisi na nazi. Familia humchagua mtu maalum ambaye anambeba mtoto huyo na kumwonesha sehemu tafauti za nyumba yao. Kila mahala anapomuonesha humwambia mfano wa maneno haya: "Hapa ni jikoni watu wanapika. Halafu humpeleka vyumbani, ukumbini na baadaye anatoka naye. Huko humpeleka katika nyumba za majirani na familia wanaokaa karibu na nyumba yao. Katika kila nyumba ambayo mtoto anapelekwa, zinatiwa pesa au zawadi yoyote ndani ya ungo. Wanaporudi nyumbani, vitu vyote ambavyo vimo ndani ya ungo hutolewa pamoja na yule mtoto. Pesa zinahesabiwa.

Halafu wazazi wanampa huyo aliyembeba mtoto zawadi yoyote na pesa kidogo.

**Wakati Wa Jioni**

Siku hiyo hiyo jioni hufanywa sherehe ya maulidi. Watu hualikwa na mtoto hunyolewa nywele au hukatwa kidogo au hakatwi kabisa. Katika baadhi ya familia mtoto hunyolewa nywele wakati wa asubuhi. Kinyozi ni mtu wa familia. Endapo hapana awezae huchaguliwa mtu mwengine yeyote. Zama za zamani mtoto alinyolewa inapofika siku ya arubaini ya uzawa wake. Nywele hizo zilipimwa kwa mizani na baadaye zilifungwa kwenye kitambaa na kufukiwa kwenye shimo.

Katikati ya maulidi mtoto huletwa na huonyeshwa. Baadaye, wengine humbeba na hurudishwa ndani. Wengine husoma maulidi mchana na watu hupewa dhifa ya pilau au biriani. Wakati mwengine maulidi yanapomalizika, watu hupatiwa vyakula vikavu kama vile keki, vileja, biskuti, juisi, soda au kahawa.

**Mtoto Anapoota Jino La Kwanza**

Mtoto anapotoa jino la mwanzo na iwapo ni mtoto wa kike, huvalishwa kidani cha fedha,vikuku vya fedha (kama bangili), na pete ya fedha. Kama familia haina uwezo wa vitu vyote viwili, anavalishwa kimoja tu. Kama mtoto ni mvulana, anavalishwa pete ya fedha au inatolewa sadaka ya pesa kidogo.

**Mtoto Anapoanza Kukaa Au Kutembea**

Zamani mtoto anapoanza kukaa mwenyewe au kutembea hulaziwa pesa kidogo chini ya mto. Ikifika asubuhi, hutolewa.

**KUMFUNDISHA MTOTO HESHIMA NA ADAB**

**Heshima Na Adabu**

Zamani, mtoto wowote aliweza kutiwa adabu na mtu mzima yeyote anayemjua na asiyemjua. Lau akifika nyumbani kwa wazazi wake na kutambuliwa kuwa aliadhibiwa kutokana na kosa fulani, wazee hao nao humtia adabu tena. Hivyo, mtoto mara nyingi aliogopa kutenda kosa nje ya nyumbani kwao. Kwa sababu alijua kuwa ataadhibiwa mara mbili. Hata hivyo, mara nyengine mtoto hakupigwa bakora. Isipokuwa mzee aliweza kumtolea jicho la hasira mtoto hadi khofu inampanda moyoni. Hayo yalifanyika hivyo kwa kuwa watu waliishi kama ndugu wa familia moja. Hawakujali rangi, kabila, madhehebu au hali na cheo cha mtu alichonacho.

Halikadhalika, watoto walifundishwa namna ya kuheshimu wazee, walimu na wakubwa zao. Pia, watoto waliweza kupelekwa kwa jirani au jamaa zake mbalimbali na kukaa huko kwa siku kadhaa. Hivyo, waliweza kujifunza akh-laki za watu wa kila namna.

Katika kumfunza heshima na adabu, mtoto alipofikia umri wa miaka mitano au sita alipelekwa chuoni (madrasa ya Kur-an).

Siku ya kwanza ya kwenda chuoni, mtoto hupelekwa na pesa kidogo, bisi na nazi ili ampatie mwalimu kama sadaka.

Halikadhalika, licha ya kusomeshwa Kur-ani, mtoto alifundishwa kazi za nyumbani. Mtoto wa kike alifunzwa namna ya kupika, kuosha vyombo, kufagia pamoja na kazi nyengine za yumbani. Naye mtoto wa kiume, alikwenda kuteka maji, kutafuta au kukata kuni pamoja na kuweka usafi wa chuo.

Jengine lililo muhimu, mtoto akishahitimu Mas-hafu' ilikuwa ni lazima itolewe sadaka. Familia ya mtoto huyo hutengeneza bisi, visheti au hutoa pesa na kupeleka chuoni.

**Watoto Kwenda Skuli**

Zamani, watoto walianza skuli walipofika umri wa miaka 6 au 7.

Skuli nyingi zilikuwa za wanawake mbali na wanaume mbali.

Elimu ya msingi ilitolewa kwa miaka minane. Masomo yaliyofundishwa ni somo la Kuandika na Kusoma, Jiografia, Historia, Kiswahili, Kiarabu, Kiingereza, Hesabu, Sayansi na Dini ya Kiislamu. Pia, walijifunza michezo kama vile netiboli kwa ajili ya wanawake na futiboli kwa wanaume. Aidha, katika skuli za wanawake, walifunzwa maarifa ya nyumbani kama kupika, kufuma, kushona, kusuka mikeka na usafi wa nyumbani. Wanaume wao walijifunza kuchora na wale wanaosoma skuli za mashamba, walifunzwa kutengeneza vikapu, mafagio na kulima.

Elimu ya sekondari wanafunzi, walijiunga mara tu baada ya kumaliza miaka minane ya elimu ya msingi. Wakati huo wa zamani, wanafunzi walisoma miaka mitatu hadi minne ya sekondari ya awali. Halafu walifanya mtihani wa nchi nzima. Wale wanaofaulu waliendelea kusoma elimu ya sekondari ya juu kwa kipindi cha miaka miwili. Hatimaye, wanafunzi waliofaulu vizuri waliendelea kusoma ngazi ya Stashahada na Shahada.

Hata hivyo, katika miaka ya zamani sana mitihani ya Zanzibar ilitungwa Chuo Kikuu cha Uingereza cha Cambredge. Wanafunzi wakifikia Darasa la Kumi na Mbili ndiyo waliyofanya mitihani hiyo na yule aliyefaulu vizuri alichaguliwa kujiunga na Chuo Kikuu cha Makerere kiliyopo Uganda.

**Adabu Ya Kula**

Zamani, watoto walikula pamoja na wazazi wao.

Watoto wanaume walikula na wazazi wanaume.

Wanawake nao walikula na wazazi wa kike. Wazee ndiyo waliyoanza kunawa mikono na kufuatiwa na watoto kulingana na rika zao.

Halikadhalika, mtoto alikuwa hana ruhusa kula kabla ya watu wazima kuanza. Aidha, alikuwa haruhusiwi kuchukua kitoweo kama vile samaki au nyama mpaka apewe.

Endapo mtoto alishiba mwanzo, hakuruhusiwa kuondoka mpaka watu wazima wanawe na kuondoka. Vyombo vilivyotumika wakati wa kula viliondolewa na watoto. Vile vile, watoto hawa ndiyo waliyosafisha mahala ambapo watu walikula.

Tabia njema nyengine ambayo watoto walifunzwa ni kumpokea mzigo mzee au mkubwa wake popote pale alipomuona. Lau mtoto huyo hamjui mwenye mzigo na wala hatambui mahali anapoishi, alitakiwa ampokee na kumsaidia japo kwa masafa fulani.

**WATOTO WAMESHAKUA WATU WAZIMA**

**Jando Na Unyago**

Jando na unyago hapa Zanibar ni mafunzo maalumu yanayotolewa kwa vijana wa kiume na wa kike waliokuwa tayari wameshafikia umri wa baleghe.

**Jando**

Ni mafunzo maalumu yanayotolewa kwa vijana wa kiume waliokuwa tayari kuuvua utoto na kuvaa utuuzima.

Umri wa kwenda jandoni kwa vijana wa kiume ilikuwa kati ya umri wa miaka 15 mpaka 18. Hata hivyo, baadhi ya makabila mengine, huanza miaka 12 au chini ya hapo.

Wakiwa jandoni, hutahiriwa na pia hupewa mafunzo ya maisha ya ndoa.

**Kutia Tohara Kutahiri**

Zamani hapa Zanzibar watoto wa kiume hutiwa tohara walipofika umri wa miaka 12 hadi18. Watoto wa familia moja au ukoo mmoja, hukusanywa pamoja na hupelekwa mbali na kwao ili kutahiriwa au kutiwa jandoni. Vijana hawa walitahiriwa na mtaalamu maalumu wa kutahiri aliyetambulika kwa jina la ngariba.

**Elimu Ya Jandoni**

Katika mafunzo waliyopewa ni pamoja na kuwaheshimu wazee, walimu wa chuoni (madrasa) na kila aliyewazidi katika rika. Aidha, walifunzwa namna ya kuwa majasiri ili wawe walinzi wa familia, vijiji, miji na nchi yao.

Mafunzo mengine waliyopata yalihusu uhusiano wa mke na mume. Hapa walifunzwa namna ya kuishi vyema na wake zao pale watapoowa kwa kuwapenda na kuwahurumia. Halikadhalika, walifunzwa umuhimu wa kushiriki katika shughuli za kimaisha kama vile kulima na kufuga ili waanze kujitegemea.

**Unyago**

Watoto wa kike waliovunja ungo ambao wanaishi mtaa mmoja au ni familia moja, walikusanywa pamoja na kupelekwa unyagoni .

**Kuvunja Ungo**

Mtoto wa kike anapopata damu yake ya mwezi (hedhi) kwa mara ya kwanza huambiwa "kavunja ungo". Mara tu damu hiyo inapochomoza hutafutwa mtu maalumu wa kumfunza msichana huyo namna ya kujinadhifisha awapo katika hali hiyo. Halikadhalika, hutakiwa ajitambuwe kuwa ameshakuwa mtu mzima na hivyo iwapo atatenda tendo la ndoa, anaweza kushika ujauzito. Mtu huyu aliyetoa mafunzo haya ya awali alitambuliwa kama 'somo' au 'kungwi'.

**Kupelekwa Unyagoni**

Zamani wasichana wakiwa unyagoni walifunzwa mambo kama vile kujiweka safi, kuheshimu wazazi, walimu na wakubwa zao. Aidha, walifunzwa taratibu zote za maisha ya unyumba. Kama vile, namna ya kujipamba, kuishi na mume kindoa, kuvaa, namna ya kuishi na wakwe zake, mawifi na jamaa mbalimbali wa mume. Baada ya kuhitimu mafunzo hayo, zilifanyika sherehe maalumu za kusheherekea tukio hilo pamoja na kuwatangaza rasmi kuwa sasa wasichana hao ni watu wazima wenye kutambua mambo.

**Hitimisho**

Maandalizi ya malezi ya watoto enzi za wazanzibar wa kale yalianza mapema mara mwanamke anapochukuwa uja uzito. Mjamzito aliandaliwa mambo maalumu kama chakula chake , nguo , sehemu maalumu ya kukaa ili ajifungue salama na kuanza kumlea mwana.

Naye mwana aliyezaliwa alikuta ameshaandaliwa mambo yanayomhusu na hupokelewa kwa dua na shangwe toka kwa wanafamilia na wengine.

Alipelekwa madrasa kujifunza kusoma kurani tukufu na elimu nyingine za maadili ya kiislamu ambazo ndizo zilizokuwa msingi mkuu wa kurekebisha maadili yake. Pamoja na haya alifundishwa kivitendo kuheshimu wengine katika jamii kwa kadri ya hadhi zao .

Alipelekwa shule kujifunza elimu za mazingira na sayansi mbali mbali pamoja na lugha za kigeni na sanaa mchanganyiko ili kumjenga kimaarifa na kumwandaa kuitumikia jamii.

Watoto walipobaleghe walipelekwa jandoni, kwa watoto wa kiume, na unyagoni kwa watoto wa kike. Huko walifunzwa namna ya kukabiliana na mabadiliko yaliyojitokeza katika miili yao na namna ya kuishi katika jamii wakiwa watu wazima tayari kuanzisha familia pindi muda utakapowadia.

Malengo makuu ya malezi haya yalikuwa kumtayarisha mtoto kuishi maisha ya maadili mema katika jamii na kutoa mchango wake kwa kadiri ya nafasi yake katika jamii husika.

**MAREJELEO**

Akida H. (1977). Utamaduni, matumizi na msingi ya lugha ya Kiswahili katika MULIKA NA. 11, TUKI Daressalaam.

BAKITA (2010) Kamusi ya Kiswahili Fasaha. Baraza la Kiswahili Zanzibar, Oxfford University Press Nairobi.

Chiraghadin S. 1974. Kiswahili na Wenyewe. Kiswahili 44:1.

Fary M.S.A (1956) Ada za Harusi Katika Unguja. Est African Literature Bureau. Nairobi.

Kanduru A. I (1988) Harusi ya Gharama. Dar-es-Salaam. Education Book Publisher.

Mohamed S.M (1972) Kiu Dar-es-Salaam. Education Books. Publishers Ltd.

Mbaabu I. (Mhar) (1985). Utamaduni wa Waswahili. Nairobi: Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Mwana Kupona (1985) Utendi wa Mwana Kupona. Ktk. Ireri Mbaabu (Mhar), Utamaduni wa Waswahili. Nairobi : Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Sengo T.S.Y. 1985.

Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini- Unguja. University of Dar-es-Salaam, Tanzania.